

**SHIRIKA LA ROZARI HAI**

**NOVENA KWA MAMA YETU WA LURDI.**
**TAREHE 02/02-10/02 /2021**

**MWONGOZO**

**1.Sali sala ya kutubu**
**2. Sali sala ya Uje Roho Mtakatifu.**
**3. Taja nia za Novena**
**3. Sala ya mwisho…Tunakimbilia Ulinzi wako**

**NIA ZA NOVENA**

**1.Tunawaombea waathirika wa Virusi vya Corona, waganga na wauguzi ili Bikira Maria wa Lurdi atusaidie na atukinge sisi na dunia nzima.**

**2. Tunawaombea watakaji wa kujiunga na Shirika la rozari hai,wanachama wa siku nyingi,watenda kazi wa Bikira Maria tuwe na udumivu na ustahimilivu ktk utume huu na kutimiza kanuni za shirika.**

**3.Tunamwombea Ustawi bora Baba Mtakatifu na kanisa lote pamoja na viongozi wa serikali, ili sauti yao iwe sauti ya Mungu.**

**4.Tunaombea wongofu wa wakosefu.**

**5.Tunawaombea Marehemu wote Toharani.**

**6.NIA BINAFSI….**

**Sala ya mwanzo.**

Ubarikiwe, ee Bikira safi sana, kwa kudhihirisha mng'ao wako kwa uhai,wema na uzuri katika Grotto ya Lurdi, huku ukimwambia mtoto Mt. Bernadeta , "Mimi ni Mkingiwa Dhambi ya Asili." Tunakupongeza mara elfu kwa kukingiwa kwao dhabi ya asili. Ee

Bikira Mkingiwa Dhambi ya Asali, Mama wa huruma, Afya ya wagonjwa, makimbilio ya wakosefu, mfariji wa wenye uchungu, unayajua mahitaji yetu, shida zetu, mahangaiko yetu, utuangalie kwa huruma. Kwa kutokea kwako kwenye Grotto ya Lurdi, ulipenda kuifanya sehemu hiyo iwe kituo kiteule cha hija, ambapo unagawa neema za Mungu. Watu wengi wamepata uponyaji katika magonjwa ya roho na mwili. Hivyo, tukiwa na Imani kamili, tunakuja kuomba kwa umama wako, utuombee tujaliwe ombi letu……… (*taja ombi lako).* Kama shukrani zetu kwa fadhila zako, tunajitahidi kuiga fadhila zako, ili siku moja tushiriki katika utukufu wako.

Ee Mama Yetu wa Lurdi, Mama wa Kristo, ulikuwa na nafasi ya pekee kwa Mwanao ulipokuwa duniani kiasi ambacho hakukukatalia chochote. Hata sasa huko mbinguni, una nafasi ile ile kwa mwanao. Utuombee kwa mwanao atujalie ombi hili maalum, iwapo kama ni mapenzi ya Mungu. Amina.
(*Sali sala ya siku husika*)

**Siku ya Kwanza.**
Ee Maria Mkingiwa dhambi ya asili, Mama yetu wa Lurdi , Bikira na Mama, Malkia wa Mbinguni, uliyeteuliwa kuwa Mama wa Neno wa Mungu kwa milele yote, ambapo kwa nafasi hii ulikingiwa dhambi ya asili, tunapiga magoti mbele yako, kama alivyofanya Bernadeta kule Lurdi na kuomba kwa tumaini kama mtoto, ili tunapotafakari kutokea kwako Lurdi kwa utukufu , uliangalie kwa wema ombi letu la sasa na utuombee tupatiwe jibu zuri kwa ombi hili tunaloliomba katika novena hii ……(*Taja ombi lako hapa*)

Ee Nyota angavu ya usafi, Maria Mkingiwa dhambi ya asili, Mama Yetu wa Lurdi, uliyepalizwa mbingui kwa utukufu, Malkia wa mbingu, utuoneshe huruma ya Mama wa Mungu, Bikira Maria Malkia na Mama, uwe faraja, tumaini na nguvu yetu. Amina.
Mama Yetu wa Lurdi, utuombee.
Mt. Benadeta, utuombee.

**Siku ya Pili.**

Ubarikiwe, ee Bikira safi sana, kwa kudhihirisha mng'ao wako kwa uhai, wema na uzuri katika Grotto ya Lurdi, huku ukimwambia mtoto Mt. Bernadeta, "Mimi ni Mkingiwa Dhambi ya Asili". Ee Maria Mkingiwa dhambi ya asili, uzimulike nyoyo zetu kwa cheche moja ya moto wa upendo wa moyo wako safi. Uzifanya zijae upendo kwa Yesu na kwako, ili tustahilishwe siku moja kufurahia utukufu wako milele. Ee mgawaji wa neema za Yesu, tunakuomba ulipokee ombi hili tunaloliomba katika novena hii na kulifikisha kwa Mwanao Yesu… (*Taja ombi lako hapa*)

Ee nyota angavu ya usafi, Maria Mkingiwa dhambi ya asili, Mama Yetu wa Lurdi, uliyepalizwa mbinguni kwa utukufu, Malkia wa Malaika na Mama, uwe faraja, tumaini na nguvu yetu. Amina.

Mama yetu wa Lurdi, utuombee.

Mt. Bernadeta, utuombee.

**Siku ya Tatu.**

"U mzuri, ee Maria, wala ndani yako hakuna doa la dhambi ya asili". Ee Maria uliyeumbwa bila dhambi ya asili, utuombee sisi tunaokukimbilia. Ee nyota angavu ya utakatifu, kama vile katika siku ile nzuri, ulivyoongea na mtoto Bernadeta pale mwambani, chemchemi ya maji ikatokea katika ardhi, miujiza ikatendeka na kituo kikubwa cha hija cha Ludri kikaanza, sasa tunakuomba uzisikilize sala zetu na kutupatia ombi tunaloliomba kwa bidiii….. (*Taja ombi lako hapa*)

Ee nyota angavu ya usafi, Maria Mkingiwa dhambi ya asili, Mama Yetu wa Lurdi, uliyepalizwa mbinguni kwa utukufu, Malkia wa mbinguni, utuoneshe huruma ya Mama wa Mungu, Bikira Maria, Malkia na Mama, uwe faraja, tumaini na nguvu yetu. Amina.

Mama Yetu wa Lurdi, utuombee.

Mt. Benadeta , utuombee.

**Siku ya Nne.**

Ee Mkingiwa dhambi ya asili Malkia wa mbinguni, sisi wanao wakosefu tunaounganisha sala zetu duni za sifa na shukrani pamoja na zile za Malaika na watakatifu wako, tukisema Utatu Mt. utukuzwe mbinguni na duniani. Mama Yetu wa Lurdi, kama ulivyomwangalia kwa huruma na upendo Bernadeta, alipokuwa anasali rozari katika grotto, utuangalie sasa kwa upendo na huruma, bondeni huku tuliko. Kutoka katika neema nyingi ulizojaliwa na Mwanao mpendwa,ee mwema Mama wa Mungu, umgawie kila mmoja wetu kile ambacho moyo wa kimama unaona anahitaji na uiangalie kwa wema neema hii tunayoiomba katika novena hii…(*Taja ombi lako hapa*)

Ee Nyota angavu ya usafi, Maria Mkingiwa dhambi ya asili, Mama yetu wa Lurdi, uliyepalizwa mbinguni kwa utukufu, Malkia wa mbinguni, utuoneshe huruma ya Mama wa Mungu, Bikira Maria, Malkia na Mama , uwe faraja, tumaini na nguvu yetu. Amina.

Mama Yetu wa Lurdi, utuombee.

Mt. Bernadeta, utuombee.

**Siku ya Tano.**

Ee Maria Mkingiwa dhambi ya asili, Mama wa Mungu na mama yetu, kutoka katika kilindi cha huruma yako. Utuangalie kwa huruma , sisi ambao kwa matumaini kamili kwa wema wako usio na mipaka na kwa matumaini kwamba Mwanao ataliangalia kwa huruma ombi lolote unalompelekea kwa niaba yetu,tunakuomba uje kutusaidia na kutuombea tupatiwe ombi tunaloliomba katika novena hii……….. (*Taja ombi lako hapa*)

Ee nyota angavu ya usafi, Maria Mkingiwa dhambi ya asili, Mama yetu wa Lurdi, uliyepalizwa mbinguni kwa utukufu, Malkia wa mbinguni,utuoneshe huruma ya Mama wa Mungu, Bikira Maria, Malkia na Mama , uwe faraja, tumaini na nguvu yetu. Amina.

Mama Yetu wa Lurdi, utuombee.

Mt. Benadeta, utuombee.

**Siku ya Sita.**

Ee Mtukufu Mama wa Mungu, mwenye nguvu sana katika nafasi yako kama Mama Yetu wa Lurdi, tunainua mioyo na mikono yetu kwako, tukiomba utuombee kutoka katika moyo mwema wa Yesu, tujaliwe msaada na neema zote za muhimu kwa manufaa ya kiroho na kimwili, pia tujaliwe neema hii maalum tunayoiomba katika novena hii…. (*Taja ombi lako hapa*). Ee Mama wa Bernadeta, ukiwa na taji la nyota za mbinguni kichwani kwako na mawaridi ya duniani katika miguu yako, utuangalie kwa wema wako vile ulivyofanya zamani zile kwa Bernadeta katika Grotto la Lurdi.

Ee nyota angavu ya usafi, Maria Mkingiwa dhambi ya asili, Mama Yetu wa Lurdi, uliyepalizwa mbinguni kwa utukufu, Malkia wa mbinguni , utuoneshe huruma ya Mama wa Mungu, Bikira Maria, Malkia na Mama , uwe faraja, tumaini na nguvu yetu. Amina.
Mama Yetu wa Lurdi, utuombee.
Mt. Benadeta, utuombee.

**Siku ya Saba.**

Ee Mungu Mwenyezi, ambaye kwa kukingiwa dhabi ya asili Bikira Maria, ulimuandalia Mwanao makao anayostahili, kwa kutafakari kutokea kwa Mama Yetu katika Grotto la Lurdi, tunakuomba kwa unyenyekevu, utujalie afya ya roho na ya mwili siku zote. Nawe Mama Maria mweye neema,mama mpenzi wa Bwana na Mkombozi wetu, utuangalie kwa wema kama ulivyofanya kwa Bernadeta siku ile na utuombee ili tujaliwe neeMa hii tunayoihitaji sana……. (*Taja ombi lako hapa*)

Ee nyota angavu ya usafi, Maria Mkingiwa dhambi ya asili, Mama Yetu wa Lurdi uliyepalizwa mbinguni kwa utukufu, Malkia wa mbinguni, utuoneshe huruma ya Mama wa Mungu , Bikira Maria , Malkia na Mama, uwe faraja tumaini na nguvu yetu. Amina.
Mama Yetu wa Lurdi, utuombee.
Mt. Benadeta , utuombee.

**Siku ya Nane.**

Ee Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili Mama wa Mungu, ulikuja kutoka Mbinguni na kumtokea Bernadeta mdogo katika Grotto ya Lurdi! Kama vile Bernadeta alivyopiga magoti miguuni pako na chemchem ya ajabu ikatokea kutoka katika ardhi ile na kama ambavyo watu wengi sana wamekuwa wakipiga magoti mbele yako ee Mama wa Mungu, tukiomba kwa huruma yako utuombee kwa Mwanao tujaliwe neema maalum tunayoiomba katika novena hii…………. (*Taja ombi lako hapa*)

Ee nyota angavu ya usafi, Maria Mkingiwa dhambi ya asili, Mama Yetu wa Lurdi, uliyepalizwa mbinguni kwa utukufu, Malkia wa mbinguni, utuoneshe huruma ya Mama wa Mungu. Bikira Maria Malkia na Mama, uwe faraja, tumaini na nguvu yetu. Amina.

Mama Yetu wa Lurdi, utuombee.

Mt. Benadeta, utuombee.

**Siku ya Tisa.**

Ee Mtukufu Mama wa Mungu, kwako tunainua mioyo na mikono yetu tukiomba utuombee kutoka katika moyo weye huruma wa Yesu, neema zote za muhimu kwa ajili ya ustawi wa roho na mwili, kwa maana ya pekee, utuombee tujaliwe neema ya kufa kifo chema. Ee Mama wa Bwana wetu wa Mbinguni, tunapomaliza novena hii, tunaomba msaada wa pekee katika hitaji letu la sasa…………. (*Taja ombi lako hapa* )

Tunaamini kuwa sala zako ukituombea, zitasikilizwa.

Ee Mama wa Bwana wangu, kwa ajili ya upendo ulio nao kwa Yesu Kristo na kwa utukufu wa jina lake, uyasikilize maombi yetu na kutupatia mahitaji yetu tuliyoyaleta katika novena hii.

Ewe nyota angavu ya usafi, Maria kingiwa dhambi ya asili, Mama Yetu wa Lurdi, uliyetukuzwa mbinguni kwa ushindi katika kuwekwa kwako kuwa Malkia wa mbinguni, utuoneshe huruma ya mama wa Mungu. Bikira Maria, Malkia na mama , uwe tumaini, nguvu na faraja yetu. Amina.

Mama Yetu wa Lurdi, utuombee.

Mt. Bernadeta, utuombee.

# TUNAKIMBILIA ULINZI WAKO……..

**Novena Hii inapatikana katika kitabu cha Sala na Novena mbalimbali cha Emilia Mkubulo.**

**Imewekwa hapa na Mratibu wa Rozari Hai**

**Fortunata Masaka.**

**Kujiunga na Utume wa Rozari tupelekee ujumbe wako whatsap kwa namba 0717 55 82 22**

**Unaweza kutembelea website yetu www.rozarihai.or.tz kupata maelezo zaidi.**